Taarifa kwa vyombo vya habari
Imezuia hadi 4 Desemba 2013 3AM

# Wananchi wadai uwajibikaji mkubwa wa wabunge

## Wananchi wengi Tanzania Bara waunga mkono madai hayo na vifungu vingine muhimu katika rasimu ya katiba

**Tarehe 4 Desemba 2013, Dar es Salaam:** Zaidi ya theluthi moja (36%) ya Watanzania Bara wameshiriki katika marekebisho ya katiba kupitia mikutano ya jamii, SMS, mahojiano, barua na barua pepe. Idadi kubwa walishiriki kupitia mikutano ya jamii iliyoandaliwa na Tume ya Kurekebisha Katiba (CRC). Pia, karibu nusu ya Watanzania Bara wanaweza kuelezea Katiba ni nini.

Matokeo haya yalitolewa na Twaweza katika utafiti uitwao: *Kurasimu Sheria Mama ya Nchi: Tafakari ya Wananchi wa Tanzania Bara kuhusu Rasimu ya Katiba*. Msingi wa utafiti huu mfupi ni taarifa kutoka *Sauti za Wananchi*, utafiti wenye uwakilishi kitaifa, uliotumia simu ya mkononi, ngazi ya kaya katika Tanzania Bara.

Taarifa zinaonyesha viwango vya juu vya ufahamu wa Katiba na ushiriki katika mchakato wa mapitio. Pia, karibu watu saba kati ya kumi (67%) ya Watanzania Bara wanafahamu kuwa rasimu ya Katiba ilizinduliwa, ingawa chini ya robo (23%) walijua jinsi ya kupata nakala ya Rasimu ya Katiba.

Moja ya maeneo makuu ya mjadala ni hali Muungano kati ya Bara na Zanzibar. Juu ya mada hii, utafiti umegundua kuwa maoni yamegawanyika, nusu (51%) wakikubali na nusu (48%) wakikataa kuanzishwa kwa Serikali tatu. Hata hivyo, walipoulizwa zaidi, idadi ya waliounga mkono Serikali tatu kwa Watanzania wa Bara, ililingana na waliounga mkono Serikali moja, wote ni 19%. *Sauti za Wananchi* pia iliweza kulinganisha matokeo haya na ya utafiti uliofanywa na Afrobarometer katika nchi nzima (pamoja na Zanzibar) mwaka 2012. Mwaka 2012 karibu nusu (47%) ya Watanzania Bara walikataa mabadiliko yo yote katika masuala ya Muungano, hata hivyo katika mwezi wa Julai mwaka 2013, robo (26%) ya Watanzania Bara walikataa mabadiliko. Kinyume chake, moja kati ya kumi (8%) waliunga mkono kuongezeka kwa uhuru wa Zanzibar mwaka 2012 wakati theluthi mmoja ya watu waliunga mkono jambo hili mwaka 2013. Utafiti wa *Sauti za Wananchi* unafanyika Tanzania Bara tu, kwa hiyo uchambuzi huu hauhusishi tawimu toka Zanzibar.

Kumekuwa na vifungu kadhaa katika rasimu ya katiba ambavyo vimekuwa vikijadiliwa kwa mapana katika vyombo vya habari. Wananchi kwa kiasi kikubwa walikubaliana na rasimu katika yote haya. Karibu wote (91%) ya Watanzania Bara wanataka kuwa na uwezo wa kumwondoa Mbunge wao kwa kushindwa utendaji, hiki ni kielelezo cha wazi cha kutaka uwajibikaji; na ni hali iliyofanya kifungu hiki kupendwa zaidi katika rasimu. Maeneo mengine ndani ya rasimu yaliyopata uungwaji mkono mkubwa toka kwa wananchi ni:

- Mgombea urais lazima awe na umri zaidi ya miaka 40 (84% wanakubaliana)
- Mawaziri na Manaibu wao wachaguliwe na Rais na kupitishwa na Bunge (77% wanakubaliana)
- Bunge lazima liundwe na wajumbe 75, wawili kutoka kila mkoa wa Tanzania Bara, wawili kila mkoa wa Zanzibari (76% wanakubaliana)

- Spika na Naibu Spika, wanapaswa wasiwe viongozi wa vyama vya siasa kwa miaka mitano kabla ya kugombea nafasi hii (72% wanakubaliana)
- Mawaziri na Manaibu wao wanapaswa wasiwe madiwani, wabunge au wajumbe wa Baraza la Wawakilishi (70% wanakubaliana)
- Wabunge wanapaswa kuwa katika ofisi kwa miaka isiyozidi 15 (70% wanakubaliana)
- Wagombea huru waweze kuwania nafasi ya Urais na Ubunge (67% wanakubaliana)
- Kuwe na tume Huru ya Uchaguzi, iliyoteuliwa na Rais (65% wanakubaliana)

*Sauti za Wananchi* pia iliwauliza Watanzania Bara kama waliunga mkono rasimu ya katiba. Pamoja na kuwepo makubaliano ya jumla katika masuala muhimu, wengi wao wangepigia kura rasimu ya sasa. Pamoja na hayo, theluthi mbili (65%) wanaamini kwamba Uchaguzi Mkuu ujao utafanywa kwa kutumia Katiba mpya.

Rakesh Rajani, Mkuu wa Twaweza, alisema *"Kimsingi, katiba inapaswa kuandikwa kutokana na maoni na amali za wananchi. Utafiti wa Sauti za Wananchi ni moja ya nyenzo muhimu inayotumika kupata maoni ya wananchi kwa njia madhubuti na ya kisayansi. Ni matumaini yetu wale waliopewa jukumu la kuandaa rasimu ya katiba watayasikiliza kwa makini."*

**---- Mwisho ----**

**Kwa maelezo zaidi:**
Risha Chande
Meneja Mawasiliano, Twaweza
**e:** rchande@twaweza.org **|** **t:** (255) (0) 656 657 559

**Maelezo kwa Wahariri**

- Taarifa hii na data zilizomo zinaweza kupatikana www.twaweza.org, au www.twaweza.org/sauti
- Twaweza ni jitihada ya miaka kumi zinazowalenga wananchi juu ya mabadiliko mapana katika Afrika Mashariki. Twaweza anaamini kwamba mabadiliko ya kudumu yanahitaji kuanzia ngazi za chini kwenda juu, na inataka kujenga mazingira na kupanua fursa za njia ambazo mamilioni ya watu wanaweza kupata taarifa na kufanya mabadiliko kutokea katika jamii zao moja kwa moja na kwa kuiwajibisha Serikali.
- Unaweza kufuatilia kazi za Twaweza kupitia:
- **Mtandao:** www.twaweza.org **Facebook:** Twaweza Tanzania **Twitter:** @Twaweza_NiSisi